# *Lakini Tangu Mwanzo Haikuwa Hivyo*

Habari za jioni, marafiki. Nina furaha sana kurejea usiku wa leo katika ibada ya Bwana Mungu. Na kutumainia baraka Zake juu ya ibada usiku wa leo.

2 Nilifurahi kuona, usiku wa leo, Ndugu Robert Daugherty nyuma chumbani kule. Ni. . .Ndugu Daugherty ndiye aliyeufadhili uamsho wangu wa kwanza. Nami ninakumbuka nikienda kwake. Bado kuna watu wengine wameketi hapa ambao walinisaidia kufika huko. Naye Ndugu Creech hapa, nafikiri, ni mmoja wao. Maono yalikuwa yameanza kutukia hivi punde, na Malaika wa Bwana alikuwa ndiyo kwanza akutane nami hapa Green's Mill, akaniambia kitakachotokea. Na haikupita majuma mawili kabla hajaniita kuja huko St. Louis. Msichana wake alikuwa na aina fulani ya ninii. . .kama ngoma ya Mtakatifu Vitus.

3 Nasi tulikuwa tumeenda kule na kuomba, na kuweka kila namna ya nadhiri, na ilionekana kana kwamba hakuna kitu kingetukia tu. Nilikuwa ninaenda kubaki tu (Maana, sikuwa nimefanya kampeni kabla ya hapo.) mpaka tu ilipokwisha, mpaka nijue kile Bwana angefanya.

4 Unajua, Ndugu Robert, ninaamini ingekuwa bora kama ningaliidumisha tu hivyo. Bila shaka, pengine kusingekuwa na wengi hivi waliookolewa. Lakini, kukaa tu na kisa kimoja mpaka kimalizike, mpaka ujue.

5 Na kesho yake, nadhani, ilikuwa ni mwendo wa saa nane au tisa alasiri, au siku iyo hiyo, sikumbuki sasa. Nami nilikuwa nimeketi kwenye gari, nje ya makazi ya kasisi. Naye baba yake alikuwepo. Nami nilikuwa peke yangu. Nilihisi Roho wa Bwana akija, nami nikatoka nje ya makazi ya kasisi na kuketi pale nje. Naye maskini Betty alikuwa tu kama mtu mkali, akipiga tu mayowe. Wala madaktari hawakuweza kumfanyia chochote. Nao mama na baba, wote wawili, walionekana wabaya sana. Walikuwa wameketi, siku na majuma, pamoja naye. Na hapo ono likaja, mbele tu ya lile gari, mbele ya lile gari. Nami nikaona lile ono, ndipo nikaingia ndani mbio na kumwambia Ndugu Robert na hao wengine la kufanya hasa. Huyo msichana atakuwa mzima.

6 Nadhani ulisema atakuwa hapa kesho usiku, sivyo, Ndugu Robert, kutoa ushuhuda? Kwa hiyo sasa kama. . .Hiyo imekuwa kama miaka kumi na minne iliyopita, nadhani, miaka kumi na miwili, kumi na minne iliyopita. [Ndugu Robert Daugherty

anasema, “Ni kumi na mitatu, naamini.”—Mh.] Miaka kumi na mitatu iliyopita. Naye ni mwanamke mchanga mwenye afya, mrembo. Atakuwa hapa kesho usiku, Bwana akipenda.

7 Uponyaji wa Kiungu hudumu mradi tu imani ingalipo, hiyo ni kweli, maadamu tu imani ingalipo.

8 Nami naamini ninamwona Ndugu Fred Sothmann, na marafiki zangu kutoka Canada wameketi hapa nyuma, pia. Nimefurahi kuwaona nyote hapa ndani usiku wa leo. Na marafiki wengine wengi hapa. Laiti ningalikuwa na wakati wa kuwatambua kila mmoja wenu. Nadhani nisingeweza, kutoka papa hapa, lakini nataka mjue kwamba bila shaka tunawakaribisha. Ndugu Boyd hapa, ninaamini ninamkumbuka. Na huyu ndugu Mmenoni. Kwa hiyo tulifurahi kuwa nanyi hapa kwenye wakati huu mdogo wa ushirika katika Neno. Na sasa, kesho ninii . . .

9 Tunataka kutangaza hili, pia, kwamba, vitabu vya hivi punde zaidi. Sasa hatuko hapa . . .

10 Siwezi kumkumbuka ndugu huyu anayeketi, ndugu Mmenoni karibu naye. Siwezi . . . [Ndugu mmoja anasema, “Harson.”—Mh.] Harson. Naam.

11 Vile—vile vitabu viko huko nyuma, kwenye meza huko nyuma. Ndizo jumbe za hivi punde zaidi. Havijawahi kuwa kwenye miamsho bado. Viko kule nyuma pamoja na kanda, jumbe za hivi punde zaidi na kadhalika. Nao hao vijana wamevichapisha, navyo vinapatikana nyuma ya jengo mnapotoka usiku wa leo. Nami nafikiri . . .

12 Asubuhi, nafikiri mahojiano yataanza kama saa mbili au saa mbili na nusu, asubuhi. Na, jamani! Nilimwambia afanye mahojiano kwa ajili ya wale waliotaka kuniona faraghani kuhusu mambo ya kiroho. Jamani, sikujua ya kwamba hii maskani ndogo hapa ingeninii . . . ingekuwa hivyo. Lakini bila shaka imekuwa na msongamano wa watu. Jamani! Kwa hivyo, vema, ni nzuri. Bwana wakati mwingine hupata baraka kutokana na kile tunachojaribu kufanya, kufanya jambo fulani kuwasaidia ndugu na dada safarini.

13 Sasa tunajaribu, kila usiku, kupata kitu ninachotafuta. Na hicho ni, kwamba, Mungu kwa ono ameniambia ya kwamba huduma yangu inafanya badiliko lake la tatu. Nami ninatamani ianzie hapa maskanini. Sijui kama itabadilika au la, lakini ninatamani ibadilike. Nami ninaamini kuwa itakuwa kwa njia ambayo itaninii . . . Nitaweza kuhubiri Injili hivi kwamba, au kufanya kitu ambacho kitasaidia wanadamu wanaoteseka wapate njia ya maisha yenye furaha zaidi, na njia ya maisha yenye afya zaidi. Ndiyo shauku yangu ya dhati. Kwa hiyo huenda ikawa usiku wa leo ambapo . . .

14 Nilimwuliza binti-mkwe wangu kuhusu kadi za maombi, naye hana zozote pale. Na Billy kwa kawaida huziweka. Wala

Gene na Leo hawana yoyote. Kwa hiyo itatubidi tu kutumia hizi ibada bila hizo, nadhani, vizuri tuwezavyo, kama tukifanya usiku wa leo. Tutaona jinsi itakavyotokea.

15 Kisha baada ya mikutano hii, mikutano yangu inayofuata itakuwa New Zealand, halafu Australia pia, na kushuka kupitia sehemu hizo za nchi.

16 Usiku wa leo, nimechagua kusoma Maandiko machache kutoka katika Kitabu cha Marko Mtakatifu, mlango wa 7, mkipenda kuifungua, kwa kuutafakari Ujumbe.

17 Na kabla hatujafanya hivyo, hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo tu na tuzungumze Naye.

18 Bwana, tunakushukuru, usiku wa leo, kwa ajili ya majaliwa ya kukutana pamoja, kwa mara nyingine. Umekuwa mwema sana kwetu kote katika siku hii. Umetupa uhai na nguvu hata tumepata nafasi ya kuja tena kwa huduma Yako na kukuabudu.

19 Nasi tunashukuru kwa ajili ya nchi yetu, kwamba bado kuna fursa na mlango wazi, kwamba wanaume na wanawake wanaweza kumwabudu Mungu kulingana na mwongozo wa dhamiri zao wenyewe. Na iendelee muda mrefu, Bwana. Lakini tunaona, kulingana na unabii wa Biblia, kwamba hivi karibuni milango hii itafungwa, duniani kote. Basi tujalie, usiku wa leo, tupokee wema wa Mungu na baraka, na Nuru yote tunayoweza, juu ya Maandiko, Bwana, ili tuwe tayari wakati saa hiyo itakapokuja, kwamba aliyehifadhiwa ndani ya nafsi zetu atakuwa ni Roho Mtakatifu, atakayeweza kufunua mambo haya niani mwetu.

20 Tungeomba hasa, usiku wa leo, pia, Bwana, kwa ajili ya wale walio wagonjwa, wahitaji, na wanaoteseka. Nguvu Zako kuu za uponyaji na rehema zitakaa juu ya kila mmoja wao. Libariki Neno Lako linaloendelea, Bwana, nasi tutakusifu Wewe. Katika Jina la Yesu, tunaomba. Amina.

21 Katika Marko Mtakatifu, mlango wa 7, tunasoma mistari michache hivi.

> *Ndipo Mafarisayo na baadhi ya walimu wa sheria waliokuwa wametoka Yerusalemu wakakusanyika mbele yake.*
>
> *Na walipoona wengine kati ya wanafunzi wake wakila mikate kwa mikono najisi, yaani,* bila kunawa, *wakawapata na makosa.*
>
> *Kwa maana Mafarisayo na Wayahudi wote wasiponawa mikono mpaka kiwiko,* hawali—*hawali, wakishika mapokeo ya wazee wao.*
>
> *Tena* wakitoka *sokoni, wasipotawadha, hawali. Na yako mambo mengine mengi waliyopokea* na *kuyashika, kama. . .kuosha vikombe, na midumu,* na sehemu za chini *na vyombo vya shaba, na meza.*

> *Basi wale Mafarisayo na waandishi wakamwuliza, Mbona wanafunzi wako hawaendi kwa kuyafuata* mapokeo *ya wazee, bali hula chakula kwa mikono* najisi?
>
> *Akajibu akawaambia,* Isaya *ametabiri vema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, Watu hawa huniheshimu kwa midomo, ila* mioyo *yao iko mbali nami.*
>
> *Nao waniabudu bure, wakifundisha* fundisho *lililo maagizo ya wanadamu.*
>
> *Ninyi mwaziacha* amri *za Mungu na kuyashika mapokeo ya wanadamu, kama kuosha midumu na vikombe: na mambo mengine mengi kama hayo mnayofanya.*
>
> *Akawaambia, Vema . . . mwazikataa* amri *za Mungu ili mpate kuyashika* mapokeo *yenu wenyewe.*

22 Na katika Kitabu cha Mathayo Mtakatifu, mlango wa 19 na kifungu cha 8, na sehemu ya mwisho ya kifungu hicho cha 8, ningependa kusoma kwa ajili ya somo. Na hivi ndivyo inavyosema:

> *. . . lakini tangu mwanzo haikuwa hivyo.*

Naye Bwana abariki kusomwa sasa kwa Maneno Yake.

23 Wakati Bwana wetu alipokuwa hapa duniani, alikutana, katika siku za huduma Yake, na watu walioshika mapokeo yao ya wanadamu, na kufundisha mambo ambayo yalikuwa kinyume na amri za Mungu.

24 Sijui, usiku wa leo, kama angekuja tena usiku wa leo, waziwazi, kama karibu asingekutana na hali ile ile. Jinsi ambavyo kwamba waliyashika mapokeo hayo kwa uchaji sana, baada ya kupokea amri za Bwana, yale tu wanayopaswa kufanya! Wanadamu hawawezi kuridhika na kile ambacho Mungu anasema kifanywe; inabidi wajipange kidogo kuhusu hilo.

25 Na mwanadamu anaposhika kitu chochote, anapotosha kitu kilicho muhimu. Na kupotosha chochote ni kukitofautisha na cha asili.

26 Kama vile, udhalimu, udhalimu si kitu ila haki iliyopotoshwa, kile akili ya mwanadamu iliyopotoshwa inachobadilisha.

27 Mungu aliwaumba wanadamu waishi kwa furaha mmoja na mwenzake. Upotovu huwabadilisha na kuwafanya kuwa maadui wenyewe kwa wenyewe. Mwanadamu anatufanya kuwa maadui sisi kwa sisi, wakati Mungu alitufanya kuwa ndugu mmoja kwa mwingine.

28 Mwanadamu aliwafanya watu kuwa watovu wa uadilifu. Mungu alimuumba mtu aishi mwaminifu kwa mke wake. Lakini mwanamume huja na kuyapotosha hayo, wala haridhiki na mke wake mwenyewe, lakini anataka kuishi na wake wengine.

29 Mungu alitupa maji safi na mazuri ya kunywa. Inambidi mwanadamu kuyachanganya na kileo ama kitu kingine, kabla hajayanywa. Ni kupotosha, kutoka mwanzo wake halisi.

30 Na kwa kufanya hivyo, tunaona kwamba katika kanisa, mambo haya yametukia, kwa sababu, mwanadamu huanza kuchezea mambo ya Mungu, naye hutoa wazo lake la vile yanayomaanisha. Yeye halichukulii jinsi tu lilivyoandikwa, bali anachanganya wazo lake mwenyewe Nalo. Halafu basi, kwa kufanya hivyo, anaanzisha mapokeo, naye anafundisha hayo. Naye Yesu alisema, alipokuwa duniani na kukutana na hayo, Yeye alisema, "Mnaniabudu bure." Sasa kuna uwezekano, basi, na ndivyo ilivyo, kwamba kunaweza kuwa na ibada ya kweli ya Mungu, isiyo sahihi. "Nao waniabudu bure, wakifundisha Mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu."

31 Sasa katika somo letu la Maandiko usiku wa leo, kama mngeendelea kusoma, mngepata jambo hilo ambapo Mungu alisema, "Waheshimu baba na mama yako; na mtu akimdharau baba yake au mama yake, kufa na afe." Lakini akasema, "Kwa mapokeo yenu mmezitangua amri za Mungu, na kusema, 'Ikiwa ndivyo, mtu akimdharau baba yake au mama yake, kwamba hiyo ni wakfu, naye atakuwa huru.'"

32 Mnaona jinsi watu wanavyopotosha mambo? Bali wanapenda kuabudu, na wanafikiri kwamba wanaabudu sawa, wakati wanaabudu vibaya. Nami nina hakika, baada ya kutokuwepo kwa Kristo, kwa miaka elfu mbili, kitu kimeenda kombo mahali fulani, kwa sababu tunapata mawazo mengi kupita kiasi.

33 Na, usiku wa leo, kuna karibu madhehebu mia tisa mbalimbali ya makanisa ulimwenguni, hayo ni madhehebu ya Kikristo, mawazo mbali mbali. Na kila moja linashikilia mapokeo yake. Loo, jinsi wanavyopenda kusema kwamba, "Mapokeo yangu ni ya kweli." Ndipo wakati. . .Kanisa moja litalielezea kwa njia fulani, na kusema, vema, kulifanya karibu kuwa kamilifu, ya kwamba kanisa hilo ni la kweli. Nasi tumepitia hilo katika siku chache zilizopita usiku hapa, kuhusu kwa nini sisi si madhehebu. Basi dhehebu linapoundwa, linaundwa kwa msingi wa mtu fulani kupata ufunuo wa jambo fulani, ambao kwa jumla unaweza kuwa ni mzuri, lakini anauundia dhehebu ndipo basi hawezi kusonga mbele zaidi.

34 Lakini Mungu anataka tukae huru. Anatutaka tufikie mahali ambapo kama akitupa Nuru, tunaweza kuipokea Hiyo, na kupata Nuru zaidi, na Nuru nyingine zaidi, na tuzidi tu

kuendelea. Ndiyo maana tunapenda kukaa huru, ili tuweze tu kuihubiri Biblia, jinsi ilivyoandikwa, na kuiamini tu hivyo.

35 Na, siku hizi, tumeingia kwenye mapokeo. Sasa, katika somo letu tunaona, usiku wa leo, ya kwamba walisema, "Je, ni halali kwetu kumwacha mke wetu kwa sababu yoyote ile?" Vema, ni karibu hivyo leo. Ikiwa hawataki kabisa kuishi na mke wao au mume wao, wao hutafuta tu sababu fulani na kumwacha. Mhubiri fulani anakuja, au hakimu, anawaoza kwa mwingine. Unaona, ni mapokeo.

"Vema," wanasema, "kanisa letu linaamini hivi."

36 Vema, haileti tofauti kubwa sana yale kanisa letu lisemayo. Ni yale Biblia isemayo juu yake, ndicho kinacholeta tofauti. Mungu anapaswa kuwa Neno la mwisho katika kila uamuzi tunaofanya.

37 Siku chache zilizopita, nilishitakiwa mahakamani, ama ningeshitakiwa. Nao walikuwa wakinipa maswali magumu sana. Nao wakasema, "Kwa nini ukapitisha pesa za miamsho kanisani mwako, kama wakfu?"

38 "Vema," nikasema, "ni kwa sababu niliambiwa na mtoza Ushuru wa Ndani kwamba ninapaswa kufanya hivyo, kwa sababu ulikuwa ni wakfu." Basi ikazidi kuendelea. Naye akasema, "Mtu huyu hakukwambia ukweli."

39 Nikasema, "Vema, aliiwakilisha serikali. Kama nikimtuma meneja wa uamsho katika mji fulani kuniwakilisha, kwa siku tano usiku huko kwenye uamsho, naye aniwakilishe siku nane usiku, ninawajibika kwa siku nane usiku, kwa sababu huyo balozi amesema siku nane usiku. Nayo serikali inapaswa kushikilia yale wawakilishi wao wanayosema."

40 Ndipo akasema, "Vema, ninii . . . mtu huyo hayuko serikalini tena."

41 Nikasema, "Na siku moja wewe hutakuwa serikalini tena. Pia walioiandika katiba hawapo pamoja nao tena. Nashangaa kama hiyo bado inashikilia." Unaona, wanajaribu kutafuta mwanya, lakini badala ya kuwa tu waaminifu na kushikilia kanuni.

42 Hivyo ndivyo watu wanavyofanya siku hizi katika nyanja zote za maisha. Hivyo ndivyo makanisa yanavyofanya; kanisa hili, makanisa mengine. Badala ya kujitokeza na kukabiliana na ukweli wa kile Mungu alichosema, tunajaribu kutafuta mwanya wa kujihesabia haki. Nayo haimpendezi Mungu. Na mtu fulani alianzisha jambo hilo, nasi tunashangaa ukweli ni upi basi.

43 Niliuliza changamoto, siku chache zilizopita, kwa mtu ambaye alikuwa amesimama na kurudia Kanuni ya Imani ya Mitume, inavyoitwa. "Ninamwamini Mungu Mwenyezi, Mungu Baba, na Muumba wa mbingu na nchi," na kadhalika, "na ninaamini katika ushirika wa watakatifu."

44 Sasa, mwanadamu hawezi kwa haki, kutoka moyoni mwake, kuikariri kanuni hiyo ya imani na kuwa sawa na Mungu, na kuijua Biblia. Chochote kinachowasiliana na watakatifu ni umizimu, chochote kinachoshirikiana na wafu.

45 Ndipo mtu huyu akageuka nyuma na kusema, "Vema, unawasiliana na nini?"

Nikasema, "Yesu Kristo."

Akasema, "Vema, alikufa."

46 "Lakini," nikasema, "Alifufuka tena. Naye hajafa, bali Yu hai. Lakini Mariamu, na mitume wengine wote, na watu wote ambao umedai kushirikiana nao, wamekufa na wametuacha. Nayo Biblia inasema, 'Hakuna mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu, ila Mwanadamu Kristo Yesu.' Kwa hiyo, pamoja na mapokeo ya wanadamu, mmezitangua amri za Mungu."

47 Nasi tunajaribu kumpendeza Mungu kwa kujenga kanisa kubwa mno, kwa kubandika viti mito, na kwa kulipamba. Hiyo ni sawa. Hakuna pingamizi kwa hilo, lakini hilo silo hasa Mungu alilosema lifanywe.

48 Tunajaribu kulifanya kanisa letu bora kidogo kuliko hilo kanisa lingine, kwa kupata mchungaji aliyeelimika zaidi tunayeweza kumpata mimbarani mwetu, ambaye anaweza kusema maneno yake kwa hotuba yenye ufasaha mkubwa. Hilo ni sawa, lakini hilo bado silo Mungu alilosema. Na katika karibu makanisa yote, ikiwa . . . Makanisa yetu leo, kama mtu hana ujuzi wa seminari, kusanyiko kamwe halitamwingiza ndani. Inambidi kuwa na elimu ya seminari. Lakini hivyo sivyo Biblia ilivyosema. Hicho sicho Yesu alichofanya.

49 Yesu aliwachukua watu ambao hata hawakujua ABC zao, na kuwatia mafuta kwa Roho Mtakatifu. Masharti ya Mungu hayakuwa kupata elimu, bali kumpokea Roho Mtakatifu. Hakuna mtu anayepaswa kuhubiri Injili mpaka amempokea Roho Mtakatifu. Mnaona jinsi tulivyozichukua amri za mwanadamu? na kuzipotosha. Yesu wa Nazareti, kabla hajawaacha wanafunzi waende wahubiri, katika Luka 24:49, alisema, "Tazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba Yangu. Lakini ngojeni, subirini kidogo tu, kabla ya kwenda. Msiruke ninapolisema. Lakini," Yeye alisema, "ngojeni katika mji wa Yerusalemu hata mvikwe uwezo utokao Juu. Ndipo mtakuwa mashahidi Wangu, katika Yerusalemu, na katika Uyahudi, na katika Samaria, na hata pande za mwisho za dunia."

50 Lakini, siku hizi, tumebadilisha hilo. Nasi tumelifanya kwamba lazima twende shuleni, na kuhitaji sarufi na saikolojia fulani, na njia fulani tunazojiendesha mi—mimbarani, na mapokeo mengi madogo madogo mbalimbali. Wala tusingeweza kuwa na mawazo finyu. Na halafu tupate fundisho la kanisa, tujifunze katekismo, yale katekismo isemayo.

51 Huokolewi kwa kujua katekismo. Huokolewi kwa kujiunga na kanisa. Huokolewi kwa kuijua Biblia. Unaokolewa kwa kumjua Yeye, Kristo. “Kwa maana kumjua Yeye ni Uzima.”

52 Kwa hiyo, twachukua mapokeo ya wanadamu, na kuzitangua amri za Mungu. Seminari zetu zinafanya hivyo. Makanisa yetu yanahitaji hilo. Makanisa yetu hayangelihitaji isipokuwa watu walihitaji. Watu hawana budi kuidhinisha hilo, la sivyo wangeweza tu kukaa mbali nalo, na kumwomba Mungu awainulie mtu fulani. Wanafanya hivyo. Watu wanafanya hivyo. Hawakulazimishi kufanya hivyo.

53 Halafu basi katika siku hizo, Mafarisayo na Masadukayo na wanadini wa siku hizo, waliamini kanisa kuwapa wokovu. Lolote kanisa lisemalo, hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa hasa, kwa maana kanisa lilisema hivyo.

54 Vema, ni vivyo hivyo tu siku hizi. Watu wanalitazamia kanisa kuwapa wokovu. Hupati wokovu kupitia kwa kanisa. Unapata wokovu kupitia kwa Kristo, si kwa kujua utaratibu fulani wa kanisa, ama kanuni fulani ya imani, ama namna fulani ya ubatizo, au—au matendo au mihemko fulani, unayopitia. Unajua na kuokolewa na Kristo, na hiyo kwa neema. Kwa imani unaokolewa, kwa wito wa Roho Mtakatifu. Hivyo ndivyo unavyomjua Yeye.

55 Lakini walikuwa nayo siku hizo, na ni zaidi sana vipi watakuwa nayo siku hizi! Ndipo watu wakaanza kushangaa, baada ya kuchukua saa kadhaa kupitia jambo hili, “Kwa nini tuko katika hali tuliyo nayo?” Hilo hapo.

56 Ikiwa kontrakta aliweka ramani kwa watu wake kujenga nyumba, *hivi-na-hivi*, na kila mtu akaipuuza ramani hiyo ya jengo, nao wakaijenga nyumba sawasawa na vile walivyodhania kila mtu anapaswa kuijenga, ingekuwa nyumba ya aina gani? Unafikiri ingepokelewa? Basi, ikiwa hivyo ndivyo, mtu mmoja angetaka ijengwe *hivi*, na mwingine *hivi*, na kila mtu angeenda na kujenga kwa wazo lake mwenyewe. Njia pekee ambayo utawahi kujenga nyumba sawa, ni kulingana na ramani ya jengo.

57 Na njia pekee ambayo tutarudi kwa Mungu na kumweka Mungu katikati yetu, ni kurudi kwenye msingi wa Biblia. Haina budi kuwa tu hivyo. Yesu alinena habari zake alipokuwa hapa duniani, na kusema, “Kwa nini mnapuuza au kuzikwepa amri za Mungu, na kuzitangua kwa mapokeo yenu?” Lakini walifanya hivyo. Na ni zaidi sana vipi wanafanya hivyo siku hizi!

58 Kwa hivyo hiyo ndiyo sababu mpangaji wa nyumba hangehamia humo. Ikiwa alibainisha aina fulani ya nyumba anayotaka kukaa, naye akatoa sheria hizo na vipimo hivyo kamili, na zijengwe hivyo, vema, kisha anazikabidhi, mjenzi anazikabidhi kontrakta. Naye kontrakta anazikabidhi msimamizi, na kadhalika. Basi kama angerudi kwenye nyumba

hii, kuhamia mle, nayo ilijengwa kombokombo, na kila njia kwa maoni ya kila mtu, asingehamia humo.

59 Basi Roho Mtakatifu anapokuja kwenye nyumba ya Mungu, hawezi kuingia ndani wakati imejengwa juu ya nadharia ya kujibunia. Haina budi kuja kwenye Biblia. Na *Hii* inapaswa kuwa ndiyo Ramani. Kwa maana imeandikwa, "Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu liwe Kweli." Sote tunataka kufikiri ya kwamba tunayo Kweli hiyo.

60 Lakini unasomaje Maandiko, kwa tafsiri ya kibinafsi? Maandiko yanasema, kwamba, "Hakuna Andiko lililotolewa kwa tafsiri ya kibinafsi ya mtu fulani." Imetolewa na Mfasiri mmoja, huyo ni Roho Mtakatifu aliyeiandika.

61 Inanikumbusha hadithi ambayo nimekuwa nikisoma alasiri hii. Ilikuwa ni maisha ya mwanzoni ya Bwana wetu, alipokuwa amezaliwa Bethlehemu na kukulia Uyahudi. Basi kwenye umri wa miaka kumi na miwili, kulikuwa na de—desturi fulani ambazo watu walizishika, hiyo ilikuwa ni sikukuu. Nafikiri Sikukuu ya Pasaka. Nao watu Wake, Mariamu, mama Yake, na Yusufu baba Yake mlezi, wote walipanda kwenda Yerusalemu kutimiza desturi hii, kihalali tu kadiri walivyoweza. Basi walipokuwa kule juu, waliingia katika njia kuu, wakizungumza na jamaa zao na kadhalika. Nao walipoondoka, wakaenda safari ya siku moja, na ndipo wakaanza kuangalia huku na huku wakimtafuta Yesu. Nao wakamtafuta miongoni mwa jamaa zao na marafiki wao, wasimpate.

62 Sijui kama hivyo sivyo karibu tu jinsi kanisa lilivyo sasa. Walipofika mahali ambapo walitambua kwamba Yeye hakuwa pamoja nao. Sijui kama kuna Mmethodisti, na Mbaptisti, na Wapentekoste, na kadhalika hapa usiku wa leo, ambao hawajafikia mahali hapo, ambapo mnatambua Yeye hayuko pamoja nanyi. Haidhuru mumefanya nini. Huenda umekuwa na njia fulani na mambo fulani ambayo ulipitia, lakini hata hivyo unajua, ndani moyoni mwako, Yeye hayupo. Sijui kama hakuna mwenye dhambi, ama aliyerudi nyuma aliye humu jengoni usiku wa leo, ambaye anatambua ya kwamba Yeye hayuko pamoja nawe, usiku wa leo.

63 Sasa, tafadhali usifanye kama Mariamu alivyofanya. Nanyi watu mnaomwabudu Mariamu, vipi kuhusu hilo? Akaanza kumtafuta. Naye akawaendea jamaa zake na marafiki zake, akifikiria angempata huko.

64 Na hivyo ndivyo wanavyofanya siku hizi. Wanaenda kanisani, kufikiri labda wangeweza kumpata mle. Mmoja anakimbilia kwenye kanisa la Methodisti, nao watagundua wanachoamini. Nao watakimbilia kwenye kanisa la Kibaptisti, na kanisa moja na lingine, wakitafuta miongoni mwa makanisa. Na wakati yote yanapohesabiwa, wanaona lundo kubwa la kanuni za imani, wala Kristo hayupo.

65 Mmoja wa watu wakuu sana katika nyanja za theolojia, nimjuaye, alikuwa nyumbani kwangu hivi majuzi. Naye akasimama chumbani. Nami nikawazia, "Mtu mkuu kama huyu angefanya nini, akija kuniona na kunitembelea?"

66 Akasema, "Ninataka tu kusema maneno machache, Ndugu Branham, kwako."

67 Nikasema, "Sawa, waweza kuketi chini?" Naye akaketi. Nami nikasema, "Ninajisikia duni sana, kuongea na mtu mashuhuri kama wewe." Naye alikuwa Rais wa Misheni kuu za Sudan, hiyo ndiyo misheni kuu sana iliyoko ulimwenguni. Naye alikuja pamoja na rafiki, aliyekuwa rafiki msiri wa Hyman Appleman. Ilikuwa ni Bw. Reidhead, huyo ndiye, Dk. Reidhead.

68 Basi akasema, "Ndugu Branham, nilipokuwa mvulana mdogo," kasema, "nilikuwa nje kondeni siku moja, nikiyaangalia mawingu yakipita mbio. Nami nikasema, 'Loo, je, kuna Mungu mahali fulani juu ya hayo?'" Kasema, "Nikamkimbilia mama yangu. Naye, akiwa mama Mkristo mzuri, alinichukua mikononi mwake na kunipenda, na kuanza kuniambia habari za Yesu. Na ilikuwa ni Yeye aliyekuwa akiniita." Ndipo akasema, "Yeye, kwa kuwa mwaminifu kwa kanisa lake, alinianzisha nikiwa na umri wa miaka saba, kujifunza habari za Yesu." "Vema," kasema, "nikiwa na hilo moyoni mwangu, nilienda katika kila shule niliyojua jinsi ya kuiendea." Kisha kasema, "Hatimaye nikapata Shahada yangu ya Sanaa. Niliwazia, nilipopokea shahada yangu, ya kwamba hakika Kristo atakuwa amesimama pale pale." Kisha kasema, "Wakati digrii ya Shahada ya Sanaa ilipowekwa juu yangu," akasema, "sikuninii. . .Wala hapakuwepo na tofauti yoyote." Akasema, "Nilipopata digrii yangu ya Udaktari, nilifikiri angekuwa pale." Ndipo akasema, "Haikuwa tofauti. Kundi tu la watu waliokuja na kusema mambo machache, na kunipa hiyo digrii." Ndipo akasema, "Ndugu Branham, nina digrii za kutosha kuukandika ukuta wako. Lakini Kristo yuko wapi?" Jambo ndilo hilo. Akasema, "Je, walimu wamekuwa makosani?"

69 Nikasema, "Ndugu Reidhead, nisingependa kusema *hivyo*: 'Waalimu wamekuwa makosani.' Kwa maana sina mamlaka ya kusema *hivyo*. Lakini hebu niseme *hivi*: Kristo haji kwa Shahada ya Sanaa au Daktari wa Uungu. Bali Yeye huja kwa kufanywa upya roho yako, kwa Roho Mtakatifu anayetoka Mbinguni."

Akasema, "Unafikiri hilo lingekuwa kwa ajili yangu?"

Nikasema, "Kulingana na Biblia hii ya kale iliyobarikiwa, ni kwa 'yeyote atakaye na aje.'"

Akasema, "Nimefundishwa kuwa hiyo ilikuwa kwa ajili ya siku zilizopita."

Nikasema, "Basi, mwalimu aliyekufundisha hivyo, alikosea."

Kasema, "Unajuaje walikuwa makosani?"

70 Nikasema, "Nimeupokea. Na Biblia iliuahidi Huo. Nitaninii. . .Hapa ndipo alipouahidi. Sasa niambie na unionyeshe mahali alipowahi kuiondoa ahadi hiyo. Alilipa Kanisa mamlaka ya kufanya hivyo. Sasa Yeye kamwe aliyaondolea wapi? Kama Kanisa likiwaambia ya kwamba mambo hayo yamepita, basi wanafundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu, wala si ya Mungu. Wanazichukua amri za Mungu na kuzitangua, kwa mapokeo yao." Hiyo ni kweli.

71 Huwezi kumpata miongoni mwa jamaa zako. Huwezi kumpata kama ukienda na kusema, "Nitakuwa Mmethodisti, kitambo kidogo, nione kitakachotukia. Nitakuwa Mbaptisti, kitambo kidogo, nione kitakachotukia." Kamwe hutampata huko, wala katika kanisa lingine lolote la madhehebu. Lakini kanisa lolote unalotaka kuingia, si dhehebu, lakini ingia katika ushirika, si kanisa kwa jumla, bali ushirika wa Roho Mtakatifu. Basi umempata. Hapo itakuwapo imani imara.

72 Kama wewe ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mkatoliki, Mpresbiteri, chochote kile ulicho, ukimpata Yesu kama Mwokozi wako binafsi, si kwa kupeana mikono na mhubiri, au mafundisho ya kanuni ya imani, bali kwa kumpata Bwana Yesu. Nayo makanisa siku hizi, yakiunda kanuni zao za imani hivyo, yanamwibia Mungu. Wanachukua mafundisho yao, na kuzitangua amri za Mungu. Halina athari kwa watu. Kwa nini? Kwa sababu theolojia yetu ya kujibunia, mafundisho yetu na kanuni zetu za imani, zimezizuia baraka zisiwafikie watu, wala hawana nafasi ya kulipokea. Hawajui lolote juu Yake. Wanajua tu kwamba wao ni wafuasi wa kanisa. Na hiyo ndiyo sababu hatuna ushirika, makanisa, moja na jingine. Hiyo ndiyo sababu kwamba wanakuwa na uamsho na makanisa mengine hayatashirikiana nao, dhehebu fulani, kwa sababu wanasema, "Sio imani yangu."

73 Kuna Imani moja tu. Biblia ilisema hivyo. Si imani katika kanuni ya imani; si imani katika dhehebu. Lakini imani katika Mungu. Hiyo ndiyo imani pekee iliyopo. "Imani moja, Bwana mmoja, na ubatizo mmoja." Maandiko yanasema hivyo.

74 Na sasa, baada ya kwenda, kusafiri siku nzima, wakitafuta miongoni mwa jamaa zao, wala wasingeweza kumpata.

75 Sijui, usiku wa leo, ni watu wangapi humu ndani wameenda kwenye kanisa la Baptisti na kashikamana na Baptisti. Sasa, hakuna kitu. . .

76 Siyapigi teke makanisa. Mimi ninaunga mkono kila moja la hayo. Lakini, ninachotetea, ni. . .ninachopinga, ni, wanaunda kanuni zao za imani, na kuchora mistari na mipaka. Kama kila kanisa lilikaa moja kwa moja kwenye Biblia, na kuisoma tu jinsi hiyo, wala lisiigeuze, liiache tu jinsi Mungu alivyoiandika, lakini watapiga hatua kidogo, waseme, "Loo, hiyo ilikuwa ni ya wakati

mwingine." Si ya wakati mwingine. Mungu ni yeye yule jana, leo na hata milele.

77 Sasa, utaenda safari ya siku moja, na utaangalia pande zote na kuona kanuni fulani ya imani, ndipo utawazia, "Vema, labda hii ndiyo." Na utaingia ndani na utaangalia pande zote. Kutakuwa na mtu humo ndani atakayefanya kitu fulani. Utasema, "Hili silo."

78 Utachukua barua yako kutoka kwa kanisa hilo na kuipeleka kwa lingine. Halafu utakuwa humo ndani siku chache, au labda majuma, au miezi, au hata miaka. Mtu fulani ataivuruga mipango yako, nawe utahamia na barua yako, mahali pengine; kisha utoke huko, uende mahali fulani. Kamwe hutulii. Biblia ilisema, "Wewe ni kama nyota zipoteazo, merikebu zisizo na matanga, zichukuliwazo na kila upepo wa mafundisho." Huku, Biblia inatukataza kufanya hivyo.

79 Kuwa imara. Jua unaposimama. Usiliwekee msingi . . . Sasa, unaweza kuwa mwaminifu kabisa kwa hilo, kuwa imara. Unaweza kuwa Mmethodisti thabiti, Mbaptisti, Mpresbiteri, Mkatoliki, ama chochote kile, imara tu. Lakini usiwe imara katika mafundisho ya kanisa lako. Uwe imara katika Mafundisho ya Biblia. Kisha chunguza mafundisho yako kwa Biblia. Uliza Yesu alikuwa nani. Kama Yeye si yule yule leo, basi fundisho lako si sahihi.

80 Unao mfano. Naye alisema, "Mimi ni mfano wenu. Nimewapa kielelezo, ili mtendeane kama Mimi nilivyowatendea ninyi." Yohana Mtakatifu 13.

81 Sasa, lakini unaona, hilo ndilo linalotukia. Sasa, kuna njia moja tu halisi ya kumpata basi, kama hangeweza kumpata miongoni mwa jamaa. Alirudi pale alipomwacha.

82 Hivyo ndivyo kanisa linavyopaswa kufanya. Rudi pale ulipomwacha, na hapo utampata, ninyi Methodisti, Baptisti, na Wapentekoste, na Assemblies of God, na ninyi nyote, Maskani ya Branham, na kadhalika. Rudini mlipomwacha.

83 Inanikumbusha juu ya kasisi wa jeshi, siku moja, kwenye Vita vya Pili vya Dunia. Alikuwa akiniambia kuwa yeye alininii kwa bombom . . . alimwendea m—mtu ambaye alikuwa . . . bombom . . . wakamwambia kuwa anakufa, alikuwa amepigwa risasi kifuani kwa bombom, risasi nyingi, naye akasema huyo mtu yuafa. Basi huyo kasisi akaingia akamwone. Naye alikuwa kapteni. Akaingia kwenye hema, naye akasema, "Kapteni, wewe ni Mkristo?"

Akasema, "Vema, wakati mmoja nilikuwa Mkristo."

Akasema, "Ndipo ikawaje?"

Akasema, "Kamwe sikumbuki ilivyoanza."

84 Naye akatazama chati yake. Ndipo akaona alikuwa amepewa tu kama dakika tatu hadi tano za kuishi, na

sehemu kubwa ya wakati huo ilikuwa tayari imetumika. Jinsi hatujui lakini muda wetu mwingi tayari umetumika pia! Basi kasisi akamwambia huyo kapteni, akasema, "Kapteni, kwani ulimwacha wapi?"

"Vema," akasema, "Siwezi kukumbuka sasa hivi."

85 Kasema, "Afadhali uharakishe, kwa maana huna muda mwingi wa kurudi nyuma safarini ulikomwachia." Kisha kasema, "Popote ulipomwacha, basi nenda pale pale uanze, nawe utampata."

86 Basi huyo kasisi alisema kwamba alingoja kwa dakika chache akiwa na Biblia mkononi mwake kusikia yale huyo kapteni angesema. Basi akaendelea kuwaza na kuwazua, akajitahidi, huku damu ikijaa pafu lake. Ndipo baada ya muda kidogo, tabasamu kubwa likamjia usoni mwake, nayo machozi yakatiririka shavuni mwake. Akasema, "Loo, nakumbuka."

Kasema, "Anzia hapo, kapteni, haraka."

87 Ndipo kapteni akasema, "Sasa najilaza kitandani. Naomba Bwana aihifadhi roho yangu. Na kama nikifa kabla sijaamka, naomba Bwana roho yangu aichukue." Akageuza kichwa chake, naye akaaga dunia.

88 Alimpata wapi? Katika ujuzi wake wa shule ya upili? Katika mafunzo yake ya saikolojia ya mwanadamu? Katika kanuni yake ya imani? Katika kanisa lake? Hapana! Alikuwa amempata wapi? Utotoni. Hapo ndipo amemwacha, na hapo ndipo Yesu anapongojea.

89 Hatutampata Yesu kwa kurudi mwanzoni mwa Ubatizo, kurudi mwanzoni mwa Umethodisti, au Ukatoliki. Tutampata Kristo tu tutakaporudi kwenye pentekoste, mwanzoni. Sio dhehebu sasa, bali kwenye tukio halisi la kipentekoste. Wakati watu mia moja na ishirini walipokuwa wamekusanyika katika Chumba cha Juu ambamo Yesu alikuwa amewatuma huko, Naye akawaambia, "Ngojeni katika mji wa Yerusalemu mpaka mtakapovikwa Nguvu zitokazo Juu."

90 Hatutawahi kusubiri muda mrefu kutosha kupata elimu ya kutosha, si kupata Digrii za Udaktari, au ujuzi wa kithiolojia. Lakini itatubidi kungoja hadi huyo Roho Mtakatifu wa kipentekoste amshukie mtu binafsi, akiwa na Nguvu za kudumu kwa mwanamume ama mwanamke huyo kugeuza uso wake kutoka dhambini na mambo ya ulimwengu, na kuishi kama Mkristo. Ndipo basi unaweza kujiunga na kanisa lolote utakalo.

91 Lakini tulimwacha kwenye pentekoste. Methodisti ilimwacha kwenye pentekoste. Baptisti ilimwacha kwenye pentekoste. Katoliki ilimwacha kwenye pentekoste. Waamishi walimwacha kwenye pentekoste. Kina Ndugu walimwacha kwenye pentekoste. Assemblies of God walimwacha kwenye

pentekoste. Kanisa la Muungano lilimwacha kwenye pentekoste. Hapo ndipo Yeye alipoanzia.

92 Ee Mungu, saidia hili liingie ndani kabisa kwenye kila moyo. Hiyo ndiyo sababu Yeye hawezi kukaa katika jengo hili. Hiyo ndiyo sababu Yeye hawezi kuja kwa kanuni zetu za imani na madhehebu. Tumeziacha zile kanuni.

93 Sikilizeni. Yesu alisema, "Mimi ndimi Mzabibu, nanyi ni matawi." Basi wakati Kanisa lilipojizika Lenyewe ndani ya Yesu, lilizaa tawi la kipentekoste. Na kama tawi la kwanza lilichipuka kwenye huo Mzabibu, la kipentekoste, itabidi kila tawi liwe kama lile la kwanza. Hatuna budi kurejea kwenye tukio la kipentekoste tena.

94 Mzabibu ukitoa tawi la mzabibu hapa, tawi linalofuata litakuwa la mzabibu, tawi linalofuata litakuwa la mzabibu, na tawi linalofuata litakuwa la mzabibu.

95 Naye Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Naye anaweza kuwa na aina moja tu ya matawi, na hayo ni matawi ya kipentekoste, Kanisani Mwake, pamoja na matukio ya kipentekoste.

96 "Loo," unasema, "Ndugu Branham, hebu kidogo. Mimi ni mwaminifu kwa kanuni yangu ya imani."

97 Kama kanuni yako ya imani inafundisha ya kwamba unachopaswa kufanya tu ni kupeana mikono na mhubiri, Yesu alisema, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo."

98 Unasema, "Ndugu Branham, mimi ni mfuasi wa dhehebu kubwa, na kanisa langu linasema kwamba siku za miujiza zimepita."

99 Yesu alisema, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Mwanzo ulikuwa wapi? Pentekoste, ambako Nguvu za Mungu aliye hai ziliwashukia watu mia moja na ishirini, na kuwabatiza kwa Roho Mtakatifu na Nguvu, wapate kumtumikia Yeye. Hiyo iliubadilisha ulimwengu uliojulikana.

100 Unasema, "Ndugu Branham, kanisa langu linaamini." Tunaona wanawake mitaani siku hizi, wakivuta sigara, wamevaa kaptura. Unasema, "Vema, mchungaji wangu hasemi lolote kuhusu hilo. Kanisa letu linasema hiyo ni sawa."

101 Lakini Yesu alisema, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Haikuwa hivyo. "Kwa wanawake, watakaovaa vazi limpasalo mwanamume, ni chukizo machoni pa Mungu."

102 Unaniambia, "Ndugu Branham, siku chache zilizopita usiku, ulihukumu kunyunyiziwa." Lakini unasema, "Kanisa langu linafundisha kwamba unaweza kunyunyiziwa, na ni sawa."

Lakini Yesu alisema, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo."

103 Unasema, "Lakini, Ndugu Branham, kanisa langu linaamini katika kumwagiliwa. Nami ni mwaminifu. Na ni kanisa kuu."

Lakini Yesu alisema, kwamba, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo."

104 Unasema, "Ndugu Branham, nimezamishwa, 'kwa jina la Baba, na kwa jina la Mwana, na kwa jina la Roho Mtakatifu.'"

105 Biblia ilisema, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Hakujawahi kuwa na kitu kama hicho. Kufuata fundisho la sharti la kujibunia na kanuni za imani!

106 Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, kwenye Kanisa la kwanza, "Tubuni kila mmoja wenu, mkabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo, kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Chochote kilicho kinyume na Hicho, hakikuwa hivyo hapo mwanzo.

107 Mnasema, "Mimi ni wa dhehebu kubwa linalosema, 'Tunazungumza mahali ambapo Biblia inazungumza, na kunyamaza mahali imenyamaza.' Nalo kanisa letu linasema, kwamba, 'Siku za miujiza zimepita.'"

108 "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Kwa maana Yesu alisema, "Angekuwa ni yeye yule jana, leo na hata milele." "Mbingu zote zingepita, lakini Neno Lake lisingepita kamwe."

109 Tunaishi katika siku ambazo wamezichukua amri za Mungu na kuzipotosha katika mapokeo ya wanadamu, lakini haikuwa hivyo tangu mwanzo. Tunayoabudu ni mapokeo ya wanadamu, wala si amri za Mungu.

110 Tulisimama hapa na macho yetu wenyewe, jana usiku, na kumwona mhubiri kipofu akipata kuona kwake, akisimama jukwaani. Nimemwona akiponya vivuli vyenyewe vya mauti, nikamwona akiwafufua watu watatu baada ya kutangazwa "wamekufa," na daktari.

Unasema huamini hilo. "Kanisa langu haliamini hilo."

111 Lakini hiyo ilikuwa kweli tangu mwanzo. Chochote kinyume sivyo, tangu mwanzo, maana Mungu ni Mungu wa Uzima, Mungu Mwenyezi, hawezi kushindwa. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Hatuwezi kumpata katika kanuni zetu za imani. Hatuwezi kumpata katika madhehebu yetu. Hatuna budi kumpata tena pale tulipomuacha.

112 Unasema, "Vema, nimempata, Ndugu Branham. Nitakwambia nilichofanya. Nilicheza katika Roho. Najua ninaye."

"Haikuwa hivyo tangu mwanzo."

"Nilinena kwa lugha, kwa hiyo ninajua ninaye."

"Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Hiyo ni kweli.

Unasema, “Nilipaza sauti, nami ninaye.”

113 “Haikuwa hivyo tangu mwanzo.” Hiyo ni kweli. Kumjua Kristo ni kuujua Utu wa Kristo, katika msamaha wa dhambi, nayo hubadilisha maisha yako.

114 Nimeona watu wakicheza, wakipaza sauti, wakinena kwa lugha, na kadhalika, na kuishi maisha ya namna yoyote. Kwa hivyo, hiyo isingekuwa ni sawa. Nimewaona wakijiunga na makanisa, kupeana mikono, kubatizwa, kupitia kila namna ya kanuni za imani, na bado wanaishi kama ibilisi. “Haikuwa hivyo hapo mwanzo.”

115 Kukutana Naye, Mtu, Bwana Yesu, kumjua Yeye kama Mwokozi wako mwenyewe, kumjua Yeye kama Mpenzi wako, “Kumjua Yeye ni Uzima.” Lakini kanuni hizi zingine za imani na kadhalika, kamwe hapo mwanzo hazikuwahi kushuhudiwa na Bwana wetu. “Enendeni ulimwenguni kote mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.” Umbali gani? “Ulimwenguni kote.” Kwa akina nani? “Kila kiumbe.” “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Huo ndio ulikuwa mwanzo. Chochote kinyume na hilo si sahihi. Hulipati katika kanuni za imani. Unalipata katika Kristo. Yeye Ndiye pekee.

Unasema, “Ndugu Branham, Biblia ilisema hapo . . . ”

116 Ilisema nini? “Kwa Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya, lugha; nao wakishika nyoka, au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru kabisa; wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.” Hivyo ndivyo Maandiko yalivyosema. Chochote kinyume na Hilo . . .

117 Unasema, “Ishara *hizi* huwafuata: yeye ni mzee mzuri; hutoa zaka zake; anatenda mema; anamtendea jirani yake haki.” Ikiwa hayo ndiyo yote yaliyohitajika, haikumpasa Kristo kufa.

118 Inahitaji tukio la kibinafsi la kupita kutoka mautini kuingia Uzimani, na kufanyika kiumbe kipya katika Kristo Yesu, pamoja na Kristo moyoni. Huyo ni Roho Mtakatifu. Hapo ndipo ilipoanzia.

119 Hao wanafunzi walikuwa watu wazuri. Walikuwa watu wenye haki. Walilipa madeni yao. Walikuwa waaminifu. Wangetoa inchi kumi na saba katika yadi; na wakia kadhaa kwa ratili; na kwenda maili moja, watakwenda mbili. Walikuwa wa kidini sana, na vivyo hivyo na hao Mafarisayo. Lakini Yesu akasema, “Mtu asipozaliwa mara ya pili, hataingia kamwe katika ule Ufalme.”

120 Hatuna budi kurudi pale tulipomwacha. Rudini mkamtafute, kwa maana kanuni hizi za imani hazikuwa hivyo hapo mwanzo. Makanisa ya kimadhehebu hayakuwa hivyo hapo mwanzo. Kwa hiyo achana tu na kila kitu na urudi mbio kwenye pentekoste, ndipo umpate Mungu wa kweli na aliye hai, ambaye huponya wagonjwa, anawatakasa wenye

ukoma, anatoa pepo, na kudai kuwa katika Biblia, yeye yule jana, leo na hata milele. Yeye ndiye Mungu wa mwanzo. Yeye Ndiye Yule asiyebadilika. Hawezi kuwa Mungu, na kuwa kitu kimoja leo na kitu kingine kesho, na kitu kingine. Hawezi kuwa asiye na kikomo na awe hivyo. Yeye ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

121 Sasa, marafiki, katika siku tunayoishi, tunapoona kwamba watu wameuharibu ulimwengu kwa mapokeo yao, wakati wameliharibu kanisa kwa mapokeo yao, wakati wameharibu akili za watu kwa mapokeo yao! Je, hatukulipitia hivi majuzi usiku, na kuona mahali lile kanisa tezi dume la kale, ama kanisa kahaba lilikuwa na mabinti, na wote wawili wanatoa, kwa Mafundisho, uasherati wa uchafu wao? Hiyo inapitia kwenye kila shirika. Wamechafuliwa.

122 Na, sasa, sisemi ondokeni kwenye madhehebu yenu. Lakini ondokeni katika kushikilia tu dhehebu hilo. Nendeni kwa Kristo. Mambo hayo ni makosa. Turudi kwenye mwanzo. Ndipo, kama tunaweza kufanya hivyo, mtamwona Kristo akiingia kwenye nyumba hiyo iliyojengwa juu ya Mwamba imara. Na humo ishara na maajabu na kila baraka ambazo Mungu aliahidi zitadhihirishwa kupitia Kanisa hilo.

Na tuombe.

123 Kabla tu hatujaingia katika maombi, huku nikiacha onyo hili zito moyoni mwako: Je, iko *kwako* kama ilivyokuwa hapo mwanzo? Kanisa ulilomo ndani yake, ni kanuni tu ya imani au dhehebu, au ni tukio linalokuletea kama ilivyokuwa mwanzoni? Ikiwa sivyo, basi sivyo. Hivi hutakuja mwanzoni basi, na kuanzia hapa? Na kuachana na kanuni za imani na madhehebu, na kumtumikia Mungu aliye hai. Kama uko hapa, usiku wa leo, na ungetamani kukumbukwa katika maombi ya kumalizia, je, unaweza kuinua mikono yako kwa Mungu, na kusema, "Nikumbuke, Ndugu Branham." Mungu awabariki, kote jengoni. Hilo ni zuri. Hilo ni sawa.

124 Haidhuru wewe ni mfuasi wa kanisa gani, dhehebu lako, inua mkono wako, useme, "Unirehemu, Mungu, mimi." Mungu akubariki. Hilo ni sawa. Mikono dazani kadhaa iko juu, kote jengoni.

125 "Nikumbuke katika maombi, ndugu, kwenye saa hii," unasema, "kwa sababu nataka kurudi kwenye mwanzo." Mungu akubariki. Mungu akubariki, wewe, wewe hapo chini, nyuma ukumbini, juu huko nje. Bwana akubariki. Mungu anaiona mikono yenu, ni mingi sana siwezi kuihesabu. Anamjua kila mmoja. Huko nyuma kabisa, mama huyo anayejaribu kuinua mikono yake huko juu kabisa kule nyuma, ubarikiwe, dada.

126 Yesu alisema, "Mnafundisha Mafundisho yaliyo mapokeo ya wanadamu, nanyi mnazitangua amri za Mungu, kwa mapokeo yenu." Na kama Yeye alisema jambo hilo katika siku hiyo, vipi

kuhusu siku hii? Turudi mwanzoni sasa. Alikuwa na nini . . . Vipi kuhusu hilo?

127 Kama lile Tawi lilitoka katika Siku ya Pentekoste, na kuleta Kanisa la aina hiyo, wakaenda ulimwenguni kote, ishara na maajabu yakawafuata kila mahali, si ishara na maajabu tunazoziita siku hizi, bali siku ile walipotoka: walihubiri kila mahali; waliwabatiza watu, mara nyingine tena, katika Jina la Bwana Yesu; wa—wakawatoa pepo; wakawaponya wagonjwa; wakapata ushindi, tangu mwanzo hadi mwisho.

128 Na kama mapokeo ya kanisa lako yamekufundisha kinyume na Hilo, hebu turudi kwenye mwanzo tulipoliacha. Na hebu tuzae hapa, usiku wa leo, washiriki wa Kanisa kama hapo mwanzo, waliokuwa na upendano wa ndugu, mmoja kwa mwingine, wakatoa uhai wao mmoja kwa ajili ya mwingine. Wanaume na wanawake wanaopendana, upendo kama huo wa Kiungu, mpaka wakaenda gerezani au mahali pa kunyongea mmoja kwa niaba ya mwingine. Hilo ndilo Kanisa asili.

Bwana awabariki, tunapoomba.

129 Mpendwa Baba wa Mbinguni, tunapokuja kwenye kufungwa kwa Ujumbe huu mdogo, usiku wa leo, nao watu wakisimama kuzunguka kuta, wakingoja, wakiegemea kwenye nguzo, na kando ya kuta, na hata nje. Nao wanainua mikono yao, ya kwamba walitaka kukutana na huyo Yesu wa hapo mwanzo. Jalia, Bwana, katika saa ii hii, wakutane Naye. Kwa maana imeandikwa, "Heri wenye njaa na kiu ya haki, maana hao watashibishwa." Idadi kubwa ya mikono, Baba. Wengi sana, singeweza kuwahesabu mara moja. Lakini Wewe unawaona wote, na unawajua wote.

130 Na imeandikwa, kwamba, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu." Wamekuwa na kanuni hizi za imani za kutosha, nao wanatambua ya kwamba hawampati Yesu humo. Kama vile Mariamu na Yusufu, inawabidi kurudi kwenye mwanzo ambapo walimwacha. Wanatamani kurudi, usiku wa leo, kwenye tukio la pentekoste, na kumpokea Roho Mtakatifu, na huko wazaliwe upya katika Ufalme wa Mungu. Basi, jalia, Bwana, ya kwamba kila mmoja wao atapokea tukio hilo, saa ii hii. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Yesu, Mwanao.

131 Na huku tumeinamisha vichwa vyetu. Sijui kama unaweza au la; ikiwa ungependa kutoka uingie katikati ya marefu haya ya kanisa, kuna nafasi ya kutembea kupitia hapa. Njoo papa hapa chini, na usimame karibu na madhabahu, na kusema, "Ndugu Branham . . . " Kama kweli unaamini hivyo.

132 Huenda nimekuwa fumbo kwenu, nyakati zilizopita. Lakini kwa kuwa jambo fulani limetukia, mamilioni kote ulimwenguni wamelipokea. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

133 "Na inaonekana kana kwamba inarudi moja kwa moja hadi mwanzo, kwenye Biblia. Sina ujuzi huo, lakini na—nawatakeni

mniombee, usiku wa leo, papa hapa madhabahuni, na kuweka mikono juu yangu. Kwa maana hivyo ndivyo walivyofanya hapo mwanzo."

134 Filipo alishuka na kuwahubiria Wasamaria. Naye alikuwa amewabatiza wote katika Jina la Yesu. Lakini Roho Mtakatifu hakumshukia hata mmoja wao, mpaka walipotuma mtu kumwita Petro. Naye akashuka na kuwawekea mikono, nao wakampokea Roho Mtakatifu.

135 Kama ungetaka maombi, na nafsi yako ikiwa imelemewa na dhambi, na hata hivyo umejaribu makanisa na mabatizo, na kadhalika, lakini haijafaulu; ukitaka kuwa, mimi niombe pamoja nawe, usiku wa leo, njoo moja kwa moja hapa juu sasa. Nitafurahia kutoa huduma yangu ya maombi kwa ajili ya yeyote wenu, nikiwa mwaminifu. Nami ninaamini ukija katika kilindi cha uaminifu wako, Mungu anayeweza kufungua macho yaliyopofushwa anaweza kuusafisha moyo mchafu. Mungu anayeweza kuwafufua wafu, kimwili, bila shaka anaweza kumfufua kiroho. Yeye anayeweza kuuhuisha mwili unaopatikana na mauti, bila shaka anaweza kuhuisha nafsi isiyopatikana na mauti. *Kuhuisha* kunamaanisha "kufanya hai." Mungu atumbukize hilo moyoni mwenu, marafiki zangu wapendwa.

136 Ninyi watu hapa, wa jiji la Jeffersonville, na New Albany, na Louisville; sijui jinsi mtakavyosimama katika Siku ya Hukumu, kwa maana Mungu amefanya kila kitu papa hapa, kwenye maskini maskani hii ndogo ya kale, nyenyekevu, iliyoharibika. Amewaponya wagonjwa. Ameonyesha ishara na maajabu. Yeye—Yeye ameleta jambo hili, Neno Lake, bila kupotosha hata jambo moja kutoka kwenye Maandiko, na kujithibitisha Mwenyewe kuwa Mungu wa walio hai.

137 Utafanyaje Mbinguni kuwa makao yako, huku unaning'inia kwenye kanuni za imani na madhehebu, dini za uwongo, na mabatizo ya uwongo, na mihemuko ya uwongo? Utafanyaje jambo hilo, wakati liko moja kwa moja moyoni mwako, mikononi mwako, kufanya uamuzi wako? Ningalikuwa mahali pako, kabla haijachelewa muda mrefu kupita kiasi, ningekuja.

138 Kwa maana, kumbuka, Yesu alinena juu ya mwanamke mmoja kutoka kwenye taifa fulani. Naye akasema, "Malkia wa Kusini atasimama Siku ya Hukumu, pamoja na kizazi hiki, naye atakihukumu, kwa maana alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili kusikia hekima ya Sulemani."

139 Mungu akubariki, dada yangu. Ukitaka tu kupiga magoti, nenda moja kwa moja pale chini. Laiti watoto wadogo wangerudi nyuma kadri wawezavyo sasa, kwa ajili ya wale ambao wangetaka kuja na kupiga magoti kwa ajili ya maombi.

140 Nitaimba aya moja au mbili tu za wimbo huu, "Nimeitia nanga roho yangu." Nami ninataka kila mtu aombe kwa uchaji,

huku tukiona kama wale wanaomtafuta Mungu wanatamani kushuka kuja na kuomba.

> . . . tia nanga roho yangu katika kimbilio la raha,
> Sitaabiri bahari zenye tufani tena;
> Tufani inaweza kuvuma juu ya kilindi cha bahari, yenye dhoruba,
> Katika Yesu mimi ni salama milele.
>
> Nimetia nanga ninii yangu . . .

141 Kama Roho Mtakatifu atakavyo, waongoze moja kwa moja madhabahuni sasa kwa ajili ya maombi.

> . . . abiri bahari zenye tufani . . .

Njoo, wewe uliyerudi nyuma.

> Tufani inaweza kuvuma juu ya kilindi cha bahari, yenye dhoruba,
> Katika Yesu mimi ni salama milele.
>
> Niangazie, Bwana, niangazie,
> Jalia Nuru kutoka kwa Mnara wa taa . . .

142 Hivyo ndivyo ilivyo, ni Neno.

> . . . angazie . . .

Unayo ikikuangazia pande zote.

> Loo, niangazie . . .

143 Hivi hutashika njia kutoka kwenye kiti chako, ushuke? Rudi kanisani mwako, popote unapotoka; bali njoo hapa ukampate kama alivyokuwa hapo mwanzo.

> Jalia Nuru kutoka kwenye mnara wa taa iniangazie.
>
> Kuwa kama Yesu, kuwa tu kama . . .

144 Ni wangapi wangetaka kuwa hivyo? Inua tu mkono wako.

> Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
> Kote katika safari ya maisha kutoka duniani hadi Utukufuni,
> Naomba tu kuwa kama Yeye.
>
> Kutoka hori la Bethlehemu alitokea Mgeni,
> Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
> Kote katika safari ya maisha toka duniani hadi Utukufuni
> Naomba tu kuwa kama Yeye.
>
> Kuwa tu kama Yesu, kuwa kama Yesu,
> Duniani ninatamani kuwa kama Yeye;
> Kote katika safari ya maishani toka duniani hadi Utukufuni
> Naomba tu kuwa kama Yeye.

145 Kama hawa, waombolezaji wapendwa, wale ambao wamehisi kusadikishwa na Roho Mtakatifu, kuwaita kwenye kikomo chao cha mwisho. Basi kumbukeni, inaweza kutokea kwa mtu mdogo zaidi humu ndani, chini ya dakika tano. Na katika saa moja kutoka sasa, kunaweza kusiwe na mtu aliye hai duniani. Inaweza kutokea. Sayansi ilisema, miaka miwili iliyopita, "Ilikuwa dakika tatu hadi usiku wa manane." Mnajua kile ambacho tumekuwa tukihubiri katika unabii. Tayari tu kutokea. Na kwa nini Shetani aendelee kukufungia tunduni, ukiwa na shaka lililo dogo sana niani mwako?

146 Sasa, ninyi hapa ambao mmenyunyiziwa, kumwagiliwa, au—au kubatizwa kwa njia zingine mbali na ubatizo wa Kikristo, hili na lijulikane kwenu.

> *Petro alipokuwa akisema maneno haya, Roho Mtakatifu akawashukia . . . wote waliolisikia lile neno.*
>
> *Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro,* maana . . . *Mataifa . . . walimwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu.*
>
> *Kwa maana waliwasikia wakinena kwa lugha, na kumtukuza Mungu. Ndipo Petro akajibu,*
>
> *Ni nani awezaye kuzuia maji, hawa wasibatizwe, watu waliompokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi?*
>
> Ndipo *akaamuru wabatizwe kwa jina la Bwana* Yesu Kristo.

147 Matendo 19, hebu niwanukulie, ninyi Wabaptisti. Nanyi sikilizeni hili kwa makini.

> *Ikawa, Apolo alipokuwa Korintho, Paulo, akiisha kupita kati ya pwani za juu, . . . Efeso:* anakutana na *wanafunzi kadha wa kadha huko,*
>
> *Akawauliza, Je, mmepokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini? . . . wakamjibu, Sisi . . .* hatujui *kwamba kuna Roho Mtakatifu.*
>
> *Akawauliza, Basi* ninyi *mlibatizwa . . . kwa ubatizo gani? Wakasema, Sisi* tumebatizwa *kwa ubatizo wa* Yohana . . .
>
> . . . akasema, Amin, Yohana alibatiza kwa toba, *akiwaambia . . . wamwamini yeye atakayekuja . . . yaani,* Yesu Kristo.
>
> Basi *waliposikia haya,* wakabatizwa tena *kwa jina la Bwana Yesu* Kristo.
>
> *Na . . . Paulo . . . akaweka mikono yake juu yao,* naye *Roho Mtakatifu akaja juu yao;* wakanena *kwa lugha, na* kumtukuza Mungu.

148 Wagalatia 1:8, Paulo akizungumza tena.

Kama nilivyotangulia kusema, ndivyo nasema tena; *ijapokuwa sisi, au malaika wa mbinguni, atawahubiri ninyi injili yoyote nyingine . . . na alaaniwe.*

149 Haidhuru ni kanuni ngapi za nuru, ni madhehebu mangapi, ni vitu vyovyote vingapi! Kama hamjabatizwa kwa Jina la Yesu Kristo, ninyi waaminio, ninawaamuru, katika Jina la Yesu Kristo, kuja kwenye kidimbwi hiki na kubatizwa. Hiyo ni kweli. Naam. Hivyo ndivyo Maandiko yanavyosema hasa. "Kwa maana hakuna Jina jingine chini ya Mbingu, walilopewa wanadamu liwapasalo kuokolewa kwalo." Haijalishi ni kiasi gani wewe . . . yale umetenda, ni kiasi gani umempokea Roho Mtakatifu, hebu turudi kwenye mwanzo. Kama umenyunyiziwa, kumwagiliwa, ama kubatizwa namna fulani, katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," ni kanuni potovu ya imani. Hakuna mtu katika Biblia aliyewahi kunyunyiziwa, aliyewahi kumiminiwa, ama kubatizwa katika jina la "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu." Hebu turudi kwenye mwanzo, nanyi mtampata. Madhabahu iko wazi, nacho kidimbwi kinangojea. Wakati tukiimba mara moja tena, "Kuwa tu kama Yesu."

Kuwa kama Yesu, kuwa kama Yesu,
Duniani natamani . . .

150 Hivi hutashika njia kuja hapa? Vipi kuhusu nyinyi waaminio? Kutakuwa na chumba wazi hapa kwa ajili yenu, baada ya dakika moja.

Kote katika safari ya maisha . . .

151 Alisema nini? "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Ukitaka kuwa kama Yeye!

. . . hadi Utukufuni
Naomba tu kuwa kama Yeye.

152 Na tuombe tena. Njoo, dada, kama unakuja madhabahuni hapa. Ni sawa.

153 Bwana Mungu, jalia liandikwe, na jalia litendeke, Bwana. Imeandikwa, basi sasa na ifanyike. Sitakuwa na hatia katika Siku ya Hukumu, kwa kusimama nyuma ya kanuni fulani ya imani ya kanisa; bali kuhubiri Injili yote, katika Nguvu za ufufuo wa Roho Mtakatifu.

154 Sasa, Bwana, utaheshimu Maneno haya, na utamtuma Roho Mtakatifu juu ya hawa, usiku wa leo, Bwana? Na uwaponye wagonjwa na wanaoteseka katikati yetu, ili watu wapate kujua ya kwamba Mungu aliyeiandika Biblia bado yuko hapa, na Yeye habadiliki, ingawa mwanadamu anajaribu kulibadilisha Neno. Lakini Yeye ni Mungu asiyebadilika, aliyesema, "Haikuwa hivyo tangu mwanzo." Na kama tukiona kile tawi la kwanza lilichokuwa, katika ule Mzabibu, tunaweza kweli kukifanya Kitabu cha Matendo kielelezo chetu kama kanisa.

155 Jalia, Bwana, usiku wa leo, ya kwamba kila mtu hapa ambaye hajamfuata Bwana Yesu, naye Yesu akithibitisha kwamba alikuwa pamoja nao, kwa ishara na maajabu ya fundisho la Agano Jipya la Kitabu cha Matendo ambacho tawi la kwanza lilitoa, jalia waanguke kwa unyenyekevu miguuni Pake na wasonge mbele, Bwana, na wampate kama alivyokuwa hapo mwanzo. Kwa kuwa hatuwezi kumpata miongoni mwa kanuni zetu za imani na madhehebu yetu, na miongoni mwa maskini mafundisho yetu dhaifu, ya siku hizi. Hatuna budi kumrudia Mungu na Biblia.

156 Wale walio hapa wamepiga magoti, wanaomtafuta Roho Wako Mtakatifu, nao wanaamini ya kwamba atawajilia, hawaweki mfano wowote ule, njia yoyote ile. Wanataka tu Roho Mtakatifu awashukie. Jalia, Mungu, kwamba mioyo yao iweze kufunguliwa wakati huu, na Nguvu za Mungu aliye hai zianguke mioyoni mwao, na kuwajaza, na kuwasamehe dhambi zao, na kuwajaza na Roho Mtakatifu. Tujalie mambo haya, Baba.

157 Sasa tukiwa tumeinamisha vichwa vyetu, mfululizo tu kwa dakika nyingine, ninaamini Mungu atatenda kwa njia kuu sana, katika dakika chache tu.

158 Kama kukiweko na wengine hapa, usiku wa leo, ambao ni wageni, nje ya mji, ambao hawawezi kurudi kwenye ibada nyingine, na yuko katika hali ya dharura. Wakati hawa wakiwa madhabahuni, wakitafuta, na kumngojea Mungu; ambao, tutaenda kuwa moja kwa moja pamoja nao, katika dakika chache. Lakini kama wako hapa katika hali ya dharura, na hawawezi kusubiri mpaka tu . . . kwa ibada nyingine, wanataka kuombewa, naomba mwinue mikono yenu, mtu ambaye hana budi kuondoka. Mmoja, wawili. Sawa. Mmoja, wawili, walio humu ndani sasa, watatu, walio humu ndani, ambao hawawezi kungoja zaidi, kwamba wao . . . hawana budi tu kwenda. Wanne. Namwona mmoja huko nyuma. Kuna watu wanne. Watano. Mmoja papa hapa. Vema, kuna watano humu ndani, usiku wa leo, ambao hawawezi kusubiri zaidi. Nashangaa, kama mnaweza, na mnaweza kusimama kwa miguu yenu; kama hamwezi, mnaweza kubebwa. Na wakati tukiwaweka watu hawa madhabahuni, ninataka, ninyi mwingie kwenye chumba hiki cha maombi, upande wa mkono wangu wa kulia hapa, watu hawa watano.

159 Wakati tukiomba tu kwamba wahudumu wa hili, walio humu jengoni, usiku wa leo, wanaoamini ya kwamba Ujumbe huu ambao nimehubiri, kwamba kanuni hizi za imani na—na mafundisho ya kujibunia, siku hizi, si ya Mungu, bali ni ya mwanadamu; na kwamba kweli tunapaswa kurudi kwenye njia ya Biblia, turudi kwenye mwanzo. Nataka baadhi ya hao wahudumu wasonge mbele na kusimama hapa pamoja nami, tunapowawekea mikono na kuwaombea watu hawa hapa, juu ya watu hawa ambao wanatafuta baraka kuu za Mungu

juu ya maisha yao. Baadhi yenu ninyi wahudumu, mkipenda, mnaoamini Huu kuwa ni Kweli muhimu sana ya Mungu. Usije kwa njia nyingine yoyote sasa. Unaona? Uwe mtu anayeuamini Huu kuwa ni Kweli kabisa.

160 Na wale sasa, wale watano walioinua mikono yao, zungukeni upande huu mwingine, kama mnaweza. Ama, njoni nyuma ya jukwaa, kama hamwezi kuingia mle, nasi tutaona kitakachotukia katika dakika chache. Pita moja kwa moja *huku,* ndugu; ikiwa watoto watarudi tu huko.

161 Na sasa hebu wale wanaokuja sasa, wapite kwa ajili ya maombi, waruhusu wapite, mkiweza, kupitia hapa.

> . . .giza
> Litageuka kuwa siku angavu zaidi.
> Basi sote na tujipe moyo,
> Kwa maana hatujaachwa peke yetu;
> Mashuaokozi inakuja hivi karibuni
> Kuvikusanya Vito nyumbani.
>
> Basi changamka, ndugu yangu, changamka,
> (Loo, changamkeni!)
> Majaribu yetu yataisha hivi karibuni,
> Wapendwa wetu tutawalaki, tutawalaki,
> Juu ya pwani ya dhahabu.
> Sisi ni wasafiri na wageni hapa,
> Tunautafuta Mji ujao,
> Mashuaokozi inakuja hivi karibuni,
> Kuvikusanya Vito Nyumbani.
>
> Mashuaokozi inakuja hivi karibuni,
> Kwa macho ya imani naiona
> Huku ikiabiri mbio majini
> Kuniokoa mimi na wewe,
> Na kutufikisha salama bandarini
> Pamoja na marafiki tunaowapenda sana.
> “Iweni tayari,” analia Nahodha;
> Loo, angalieni, iko karibu kuwasili.

162 Tazama mabomu ya atomiki, unaweza kujua iko karibu kuwasili.

> . . .loo, changamkeni,
> Majaribu yetu yataisha hivi karibuni,
> Wapendwa wetu tutawalaki, tutawalaki,
> Juu ya pwani ya dhahabu.
> Sisi ni wasafiri na wageni hapa,
> Tunautafuta Mji ujao,
> Mashuaokozi inakuja hivi karibuni,
> Kuvikusanya Vito Nyumbani.

163 Sasa, marafiki, wahudumu hawa watakusanyika hapa sasa, karibu na hapa. Ninawaendea wagonjwa hawa wa dharura ambao hawawezi kurudi. Na sababu ya sisi kufanya hivi, kama

tufanyavyo usiku wa leo, ni kwa kuwa kuna ibada ya ubatizo inayokuja baada ya dakika chache. Nayo ibada inayofuata ya ubatizo itakuwa Jumapili asubuhi, baada ya shule ya Jumapili. Hilo litatuachia Jumamosi usiku, Ijumaa usiku, na Jumamosi usiku, na Jumapili usiku, kwa ajili ya mstari wa uponyaji.

164 Tunataka kuweka wokovu wa Mungu kwanza. Mnaona? Uponyaji utafanyika. Hatuna hofu juu ya hilo. Na kwa hiyo itafanyika. Jana usiku, Mungu aliwaokoa watu wanane wa thamani hapa madhabahuni. Loo, jinsi nilivyofurahi kuona hilo! Wala sijui hawa ni akina nani hapa. Baadhi yao wanaweza kuwa wenye dhambi, wakiita. Baadhi yao wanaweza kuwa wanamtafuta Roho Mtakatifu.

165 Lakini sasa ninaingia. Na mke wangu kule nyuma, mpenzi, kuna wanaume na wanawake mle ndani. Ninaingia tu kuona kitakachotokea. Ninaamini kwamba hiyo huduma mpya itahudumiwa humo. Mungu anajua nimesema Neno kweli kadiri nijuavyo, katika Biblia. Hiyo ni kweli. Nami ninarudi kuona kile Mungu atakachofanya.

166 Sasa, kesho usiku, Bwana akipenda hatutakuwa na ibada ya ubatizo, isipokuwa iwe ni dharura, mtu fulani anataka kubatizwa. Lakini mara moja, katika dakika kumi au kumi na tano zijazo, ibada ya ubatizo itakuwa ikifanyika.

167 Ndipo basi, kesho usiku, kutakuwa na . . . Nataka kumwuliza da-. . .yangu, binti-mkwe wangu hapa ndani, (Dada-mkwe? Huh!), binti-mkwe wangu, kama alipata kadi za maombi, leo. Loyce, ulizipata? Hakuzipata. Vema, tutaandika zingine. Tutapata zingine, kwa njia fulani. Nasi tutatoa, tutasambaza kadi za maombi, kesho usiku, Bwana akipenda, na kuanzisha mistari yetu ya maombi tukizunguka, mstari wa maombi wa mtindo wa kawaida, kama jambo fulani halitendeki katika dakika chache, chumbani. Ndipo basi tutaona. Kesho usiku, Bwana akipenda, tutasambaza kadi za maombi, mapema, kesho usiku, yapata thenashara, nadhani, ama kitu kama hicho, thenashara ama thenashara na nusu, kitu fulani, kesho usiku, ili watu wapate kadi ya maombi na kuingia mstarini.

168 Sasa, sasa hivi, ninataka kila mtu anayeweza, azame katika maombi kabisa. Nawatakeni ninyi wahudumu muwazunguke hawa watu. Lakini, Ndugu Neville hapa jukwaani. Nami nitaingia kuwaombea wagonjwa. Bwana awabariki.

169 Nanyi ndugu sasa nendeni moja kwa moja walipo watu hawa sasa. Pandeni, wawekeeni mikono, na hebu tufanye maombi, mnapozunguka. Kila mmoja wao akae nao moja kwa moja sasa, mnapozunguka moja kwa moja. Kusanyiko lote linalojua kuomba, inamisheni vichwa vyenu huko nyuma, na mumwombe Mungu kabisa, kwamba Roho Mtakatifu atawashukia hawa na kuwajaza na Roho Mtakatifu; na atafanya miujiza katika chumba hiki, kuwaponya wagonjwa na wanaoteseka.

58-1002 Lakini Tangu Mwanzo Haikuwa Hivyo
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org